

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kutoa taarifa fupi kwa niaba ya Serikali kutokana na tukio la kusikitisha ambalo limetokea Mwanza jana siku ya tarehe 18 Mei, 2016. Tukio hilo lilitokea wakati wa saa 2.35 usiku ndani ya Msikiti unaoitwa Masjid Rahman ambao unamilikiwa na BAKWATA ambao upo katika eneo la Mapankini, Mtaa wa Ibanda Relini, Kata ya Mkolani, Mkoani Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tukio hilo, watu watatu waliuawa kwa kukatwa mapanga na mashoka sehemu mbalimbali za miili yao na mmoja kujeruhiwa sehemu ya kichwani baada ya watu wapatao takribani 15 kuvamia msikitini. Watu hao waliuawa wakati walipokuwa wanaswali swala ya *Insha* ndani ya msikiti huo. Walikuja wauaji hao wakavamia msikiti wakiwa wamejificha kwa mavazi ambayo yalikuwa yanaficha sura zao. Walizima taa na kuanza kuwakata kwa mapanga na kumjeruhi mtoto mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliouawa katika tukio hilo ni Ndugu Feruzi Ismail Elias ambaye ana miaka 27 ambaye ndiye aliyekuwa Imamu wa Msikiti huo, mkazi wa Ibanda Relini. Mwingine ni Ndugu Mbwana Rajabu ana miaka 40, yeye ni mfanyabiashara na mkazi wa Ibanda vilevile na mwingine ni ndugu Khamis Mponda miaka 28 ni dereva, pia ni mkazi wa Ibanda, Mkolani. Aliyejeruhiwa ni mtoto ambaye ana miaka 13 anaitwa Ismail Abeid ambaye ni mwanafunzi wa shule iitwayo Jabal.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali, kwanza tunaomba kuchukuwa fursa hii kuwapa pole familia ya Marehemu, ya mtoto aliyejeruhiwa pamoja na Mbunge wa Jimbo la Nyamagana, Mheshimiwa Stanslaus Mabula pamoja na Watanzania wote kwa ujumla kwa msiba huo mzito, kutokana na tukio la kinyama ambalo limefanywa na watu wasio na chembe ya ubinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii vilevile kuwajulisha kuwa Jeshi la Polisi limeshaanza kufanya upelelezi juu ya tukio hili na kazi hiyo inaendelea vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie wananchi kupitia Bunge lako Tukufu kwamba damu za watu hawa waliouawa kikatili hazitapotea bure. Serikali haitolala mpaka wahusika watiwe mkononi na kuchukuliwa hatua za kisheria. Kwa kupitia Bunge lako hili Tukufu, naliagiza Jeshi la Polisi kuhakikisha linafanya kila linalowezekana mpaka wahusika wote wapatikane. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mwisho nawaomba Waheshimiwa Wabunge, wanafamilia na wananchi wote kwa ujumla kuwa na moyo wa subira katika kipindi hiki kigumu na waendeleo kuwa na imani kwamba Serikali

inalishughulikia tatizo hili pamoja na matukio mengine ya aina kama hii ya kinyama kuzuia yasijitokeze tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naomba kuwasilisha.